




PARTICIPATORY PLANTATION FORESTRY PROGRAMME

Mwongozo wa Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) Katika Mashamba ya Misitu ya Kibiashara



United Republic of Tanzania
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES
AND TOURISM**
Forestry and Beekeeping Division



Embassy of Finland
Dar es Salaam



Participatory Plantation Forestry Programme (PFP 2)

Mwongozo wa Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) Katika Mashamba ya Misitu ya Kibiashara

Februari, 2023 Iringa, Tanzania

Toleo la Ripoti: Februari, 2023



United Republic of Tanzania
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES
AND TOURISM**
Forestry and Beekeeping Division



Embassy of Finland
Dar es Salaam

Participatory Plantation Forestry Programme (PFP 2)

Rasimu ya Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) Katika Mashamba ya Misitua ya Kibiashara

Waandishi wa Ripoti:

Tiaan Pool, Iringa - Tanzania

Wachangiaji Wengine:

Andrew Ferdinands, Ida Herdieckerhoff, na Timu ya Usimamizi wa Mradi

Nukuu inayopendekezwa:

Mradi wa Panda Miti Kibiashara (PFP2) (2023). **Rasimu ya Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) Katika Mashamba ya Misitua ya Kibiashara. Iringa, Tanzania.**

Participatory Plantation Forestry Programme (PFP 2) – Panda Miti Kibiashara

Plot No. 21, Kitalu 1, Kanda 1A

Gangilonga

S. L. P. 2244, Iringa.

www.privateforestry.or.tz

Yaliyomo

DIBAJI	iv
1. UTANGULIZI	1
1.1 Usuli	1
1.2 Mambo muhimu kuhusu UJM katika Mashamba ya Misititu ya Kupandwa.....	2
Katika UJM	2
1.2.1 Ulinzi/Kujitayarisha.....	2
1.2.2 Kuzuia.....	6
1.2.3 Kuzima	7
1.2.4 Ukarabati	10
1.2.5 Utafiti.....	10
2. UCHAMBUZI WA MAENEO HATARISHI ya moto	11
3. MAJUKUMU NA WAJIBU WA VIONGOZI WA SERIKALI	12
3.1 Majukumu ya Serikali ya Kuu	12
3.2 Majukumu ya Serikali ya Mkoa	12
3.3 Majukumu ya Serikali ya Wilaya	12
3.4 Majukumu ya Serikali ya Kata	13
3.5 Majukumu ya Serikali ya Kijiji.....	13
4. MAELEZO YA MWISHO.....	14
REJEA.....	15

Orodha ya Viambatanisho

Kiambatanisho 1. Mifumo ya Usimamizi Jumuishi wa Moto	vi
---	----

Ordona ya Majedwali

Jedwali 1: Vifaa muhimu vinavyopendekezwa kwa ajili ya Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji	4
Jedwali 2: Mpangokazi wa Kijiji wa kuzima moto.....	9

Orodha ya Vifupisho

FDI	Mfumo wa Kielelezo cha Hatari ya Moto
KKMK	Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji
KUMK	Kamati ya Usimamizi wa Moto ya Kijiji
MMK	Mfuko wa Moto wa Kijiji
MUMK	Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji
MMMM	Mratibu wa Moto wa Msituni wa Mkoa
UJM	Usimamizi Jumuishi wa Moto
MMMH	Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri

DIBAJI

Rasimu ya Kijitabu hiki cha Maagizo ya Usimamizi wa Moto wa Misituni (UJM) kwa ajili ya Mashamba ya Misitu ya Kibiashara inapaswa kuzingatiwa kwa pamoja na machapisho mawili yanayoambatana. Machapisho hayo ni: **1) Sheria Ndogo za Kuzuia na Usimamia Moto (KUM) za Halmashauri za Vijiji/Mtaa; na 2) Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) cha Kidete.**

Nyaraka hizo kwa pamoja zinatoa maelekezo ya utekelezaji wa UJM, mfumo wa kisheria wa UJM na mfano wa utekelezaji wa MUMK ambao utakuwa rejea ya kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Moto kwa vijiji vyote vinavyoshiriki katika UJM.

Serikali Kuu pamoja na serikali za Mikoa na Wilaya nchini Tanzania zimedhamiria kupunguza hasara inayotokana na uchomaji moto misitu. Kwa sababu hiyo, zimeamua kwamba utekelezaji wa Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) kuwa moja ya vipaumbele vyao (Macric, na Lyimo, 2019).

Katika ngazi ya Kitaifa ya "Usimamizi Jumuishi wa Moto (UJM) - Andiko la Mwongozo wa Mashamba ya Misitu ya Kibiashara" lilitayarishwa kwa kuzingatia mienendo ya moto wa misitu, sera zilizopo za Kitaifa ikiwa ni pamoja na sera ya Misitu iliyopitiwa hivi karibuni, mapendekezo ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), na ongezeko la uwekezaji kibiashara katika misitu midogo, ya kati na mikubwa nchini (Macric, na Lyimo, 2019).

Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania walifanya majaribio ya kuanzishwa kwa UJM katika Kijiji cha Wino na Vijiji vya jirani na kufanikiwa kuweka mwanzo mzuri wa kupanga utekelezaji mkubwa wa jambo hili Kitaifa. Aidha, baadhi ya makampuni binafsi yamekuwa yakishirikiana na wananchi kutoka Vijiji vya jirani katika kuvifanyia kazi baadhi ya vipengele vya UJM, ijapokuwa siyo kwa ukamilifu na usanifu unaotakiwa. Jambo la faraja ni kwamba, serikali za Mikoa na Wilaya zimezidi kutoa uongozi na uratibu katika kupunguza uharibifu wa moto.

Usimamizi Jumuishi wa Moto unaweza kufafanuliwa kama mbinu ya kushughulikia matatizo na masuala yanayoletwa na moto unaoharibu na wenye manufaa ndani ya mazingira ya asili na mifumo ya kijamii na kiuchumi ambamo hutokea, kwa kutathmini na kuweka wiano kati ya hatari zinazoletwa na moto na manufaa ya moto huo. Au neno UJM linaweza kufafanuliwa kwamba ni majukumu muhimu ya kiikolojia na kiuchumi ambayo yanaweza kutekelezwa katika kila eneo la uhifadhi au mandhari (Myers, 2006). ITTO inaongeza kuwa UJM inajumuisha mbinu na utaratibu wa usimamizi wa moto wa misitu. Pia inajumuisha juhudi za kijadi za kuzuia moto na kuzima moto pamoja na matumizi ya moto ulianzishwa kama zana, ushirikishwaji wa jamii, na utekelezaji wa sheria za misitu.

Hata hivyo, dhana ya UJM imebadilika zaidi katika miongo miwili iliyopita na mara nyingi inatafsiriwa tofauti kidogo na watu binafsi kutokana na taaluma mbadala za matumizi ya ardhi. Kwa kawaida, tofauti za tafsiri huhusishwa na mazoea tofauti ya matumizi ya ardhi kama vile misitu ya kibiashara, kilimo na uhifadhi.

Kwa muktadha huu, UJM inaweza kufupishwa kama mbinu ya kimfumo na ya jumla ya kudhibiti moto wa nyika. Fasihi kwa ujumla hufafanua UJM kwa kuzingatia vipengele vitano vya kimkakati. Mikakati hiyo pia ina mada na shughuli mbalimbali (mbinu za utekelezaji) kwa kuzingatia vipengele vya kimazingira, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutawala. Mambo ya kimkakati ya UJM ni:

- Ulinzi / utayari (utayari wa kukabiliana na moto);
- Kuzuia (kupunguza hatari / kuzuia moto kuwaka);
- Kuzima (mwitikio katika moto/mikakati na mbinu za kuzima moto);
- Ukarabati wa maeneo yaliyoharibiwa na moto; na

- Utafiti (ukusanyaji na uchanganuzi wa takwimu unaolenga kupata suluhu ya changamoto zitokanazo na moto katika eneo husika na ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya masuala ya kitaaluma).


Rejea Kiambatanisho cha 1 kuhusu muhtasari wa mifumo ya Usimamizi Jumuishi wa Moto.

UJM inapaswa kuungwa mkono katika nyanja zote za kiutawala yaani kuanzia Serikali Kuu, Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Iwapo utashi wa kisiasa na uungwaji mkono katika nyanja zozote kati ya hizo hapo juu hautakuwepo au utakuwa dhaifu, uwezo wa mfumo wa UJM utakuwa mdogo.

Changamoto zingine ndani ya mfumo wa UJM ni pamoja na kuvunjika kwa mawasiliano kati ya wahusika, kushindwa kuboresha matumizi ya rasilimali zote zilizopo (ikiwa ni pamoja na rasilimali watu ndani ya jamii), na kushindwa kupanua wigo wa ushirikiana kwa kuvuka mipaka ya Vijiji na Vijiji. Mafanikio ya utekelezaji wa UJM yanategemea ushirikiano wa karibu na kujenga uwezo miongoni mwa wadau mbalimbali.

Kufuatia matokeo mabaya ya musimu wa moto wa mwaka 2021, wadau wakuu walikutana mnamo mwaka 2022 ili kukusanya taarifa za msingi ambazo zilisaidia kufahamu ukubwa wa tatizo la moto katika misitu na hatimaye, kuanzisha mfumo wa Usimamizi Jumuishi wa Moto kama njia ya kupunguza madhara ya moto katika Mashamba ya Misitu ya Kibiashara. Hivyo basi, waraka huu unatoa maelekezo ya uendeshaji wa UJM katika Mashamba ya Misitu ya Kibiashara.

Kiambatanisho 1. Mifumo ya Usimamizi Jumuishi wa Moto



1. UTANGULIZI

1.1 Usuli

Sekta ya misitu imekuwa moja ya vichocheo vikubwa vya uchumi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa hadi asilimia 70 ya sekta hii inayokuwa kwa kasi inashikiliwa na wakulima wa miti wadogo na wa kati pamoja na wawekezaji wazawa wanaotoka nje ya vijiji hivyo, huku Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na makampuni makubwa yakichangia sehemu iliyobaki. Wadau wa sekta hii ya misitu kwa pamoja wanachangia sehemu kubwa ya mapato ya serikali za mitaa.

Utekelezaji wa mfumo UJM Tanzania katika mikoa yenye mashamba ya miti ya kupandwa ni kazi yenye changamoto nyingi. Hata hivyo, kuahirisha utekelezaji wake kwa sasa sio chaguo sahihi. Madhara ya uharibifu wa moto katika uchumi wa maeneo hayo, ustawi wa kijamii wa watu na uharibifu wa mazingira ya asili ni dhahiri na yasipoangaliwa, yataendelea kuzuia maendeleo na ustawi wa maeneo husika.

Ulimwenguni kote, siku zilizo na hali ya hewa hatarishi kwa moto zinakabiliwa na ongezeko la idadi ya moto wenye madhara. Aidha, ukubwa wa wastani wa maeneo yaliyoharibiwa na moto usiohitajika umeongezeka katika miaka ya hivi karibuni.

Wakulima wadogo wa miti hupanda miti katika mashamba makubwa na madogo yenye ukubwa wa wastani wa chini ya hekta moja. Wawekezaji wa nje pia wameanzisha mashamba makubwa ya miti katika maeneo haya. Katika baadhi ya sehemu, mashamba makubwa na madogo ya miti huonekana kama eneo la ukanda mkubwa uliopandwa miti yenye mwendelezo. Lakini katika baadhi ya sehemu, mashamba madogo ya miti yamepandwa mtawanyiko ndani ya maeneo ya mashamba ya kilimo.

Kwa bahati mbaya, moto wa nyika umekuwa tishio kubwa kwa rasilimali hii muhimu. Kwa mfano, mwaka 2021 mashamba yenye thamani ya mabilioni ya fedha za Kitanzania yaliteketea kwa moto.

Katika ukanda huu wa Nyanda za juu kusini mwa Tanzania, wanavijiji hutumia moto kuandaa mashamba yao kwa ajili ya kupanda. Aidha, moto pia hutumika kwa ajili ya kuchoma mkaa, kuchoma matofali, kuwindia wanyama, kurina asali, kupunguza viwako msituni, na kuboresha marisho ya wanyamapori na wafugwao. Kwa hakika, moto unapotumiwa kwa uwajibikaji ni chombo kinachofaa kwa wakulima, lakini unapotumiwa kwa wakati usiofaa au bila ulinzi wa kutosha, unaweza kuenea kwa haraka na kusababisha uharibifu mkubwa.

Uharibifu wa misitu kwa kuchomwa moto umechangiwa na masuala kadhaa yakiwemo udhibiti duni wa uchomaji moto, mabadiliko ya hali ya hewa kwa ujumla, ukosefu wa rasilimali, wingi wa viwako vilivyopita kiasi kutokana na usimamizi mbovu wa misitu (kama vile kupunguzia miti shambani, kupogolea matawi, palizi na kutokuwepo kwa barabara za kuzuia moto, nk), na ugumu wa jamii kukabiliana na mabadiliko ya mazingira ya moto.

Changamoto katika sekta hii ya misitu siyo tu kwamba inatokana na ukubwa wa kazi yenyewe, bali pia ukosefu wa uwezo miongoni mwa wadau. Hivyo basi, utekelezaji wa UJM wenye mafanikio utahitaji mipango makini, kutafuta fedha za ziada ili kusaidia juhudi za usimamizi, na kujenga uwezo. Aidha, mafanikio ya Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) yatategemea iwapo mipango hiyo itapitishwa na kuwa sehemu ya mipango ya muda mrefu wa serikali kuu na serikali za mitaa.

UJM unapaswa kutekelezwa kwa kubainisha mambo muhimu ya mafanikio na kuongeza juhudi za usimamizi, na kuweka mkazo mkubwa katika mambo haya.

Ikumbukwe kwamba, Tanzania licha ya kuwa na historia yenye changamoto za hapa na pale, lakini ina urithi wa mafanikio. Maendeleo ya uchumi, mfumo wa elimu na miundombinu ya nchi katika miongo ya hivi karibuni ni ushuhuda wa uongozi dhabiti wa taifa, mtazamo chanya na uvumbuzi.

Zaidi ya hayo, kuna watu wengi wenye uwezo na ujuzi wa kuhamasisha ambao, ikiwa wataweka mawazo yao kwenye kazi, bila shaka wataweza kuzuia madhara ya uharibifu wa moto usiohitajika.

1.2 Mambo muhimu kuhusu UJM katika Mashamba ya Misisitu ya Kupandwa

Katika UJM, hatua na shughuli zifuatazo zimetambuliwa kama sababu muhimu za mafanikio ya muda mfupi na hivyo basi, zinapaswa kushughulikiwa kama suala la kipaumbele. Kwa Kuwa Tanzania ina uwezo wa kushughulikia masuala haya, hilo ni jambo la msingi katika kuleta mabadiliko ya kimaendeleo yanayokusudiwa katika UJM.

1.2.1 Ulinzi/Kujitayarisha

Ulinzi wa moto unaweza kufafanuliwa kama kuanzishwa kwa miundombinu, zana/vifaa, sheria, mawasiliano, mifumo, sheria ndogo za kuzuia na kusimamia moto na hatua zingine zinazohitajika katika kulinda maisha ya binadamu, mali na mazingira kutokana na athari mbaya za moto wa nyika.

Kwa muktadha huu, shughuli zinazolenga utekelezaji wa mifumo na uanzishwaji wa miundombinu zitasaidia kupungua kwa kasi ya kuenea kwa moto na hasara itokanayo na uharibifu huo. Shughuli hizo ni pamoja na :

Mfumo wa Kielelezo cha Hatari ya Moto (FDI)

Mfumo wa FDI ni mkusanyo wa uchunguzi wa hali ya hewa na uchanganuzi wa takwimu hizo ili kutoa tathmini ya wakati halisi na utabiri wa hatari ya moto. Tathmini na utabiri huu ni lazima uendane na tathmini za mahali hapo kutoka kwa wasimamizi wenye uzoefu. Ingawa njia hii ina dosari, lakini ina usahihi wa $\pm 70\%$ na inatumika kama mwongozo ambao unaweza kutumiwa na wasimamizi wa moto kubainisha tabia ya moto. Hivyo basi, shughuli za uchomaji zilizopangwa ni sharti zierendane na FDI na FDI, itaongoza matumizi ya moto ya siku zote.

Maafisa Watendaji wa Vijiji na Maafisa wengine walioidhinishwa watazingatia FDI wakati wa kutoa vibali vya kutumia moto. FDI inapaswa kuhesabiwa kila siku lakini pia inaweza kutumika kama mfumo wa onyo la mapema ikiwa hali ya hewa iliyotabiriwa kwa muda wa siku mbili zifuatazo itajulikana. Hii itarahisisha upangaji wa shughuli za uchomaji moto na kuongoza utoaji wa vibali vya kutumia moto.

Mfumo mzuri wa mawasiliano kati ya Vijiji, Wilaya, Vijiji jirani na wahusika wengine

Kubadilishana taarifa, kutoa maelekezo ya kazi na kuwasilisha ripoti ni shughuli muhimu sana za mawasiliano zinazohitajika kwa ajili ya ufanisi wa shughuli za UJM. Hata hivyo, njia za mawasiliano zinazotumiwa kupeleka habari zinapaswa kuwa rahisi lakini zenye ufanisi mkubwa. Mawasiliano yanaweza kufanywa kupitia mikutano, simu za mkononi, mifumo ya kengele, mawasiliano ya kibinafsi na wamiliki wa mashamba pamoja na mabango.

Kamati ya Usimamizi wa Moto ya Kijiji (KUMK) ni lazima iwe na mikutano ya kila mwezi wakati wa msimu wa moto ili kujadili na kutoa taarifa juu ya masuala yote ya usimamizi wa moto Kijijini. Pia, mkutano wa pamoja kati ya KUMK, viongozi wa Vijiji vya jirani na wamiliki wa mashamba ni lazima ufanyike mwanzoni mwa msimu wa moto ili kujadili maslahi ya pande zote ikiwa ni pamoja na maandalizi ya barabara za mipakani za kuzuia moto.

Pia, KUMK itapaswa kuandaa taarifa ya kila mwezi ya shughuli za usimamizi jumuishi wa moto Kijijini na kuiwasilisha kwa Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri (MMMH) kupitia mchakato wa kiutawala wa Halmashauri.

Mwenyekiti wa KUMK na wanachama wengine wawili wa KUMK wenye uwezo mzuri wa kutumia simu janja wanapaswa kuwezesha ili wawe na uwezo wa kupata taarifa ya FDI ya kila siku na baadaye kuisambaza kwa Wajumbe wa KUMK na Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji (KKMK), Viongozi wa Kijiji na wanakijiji kwa ujumla.

Ubao wa FDI unaoonyesha ukadiriaji wa kila siku wa FDI unapaswa kujengwa katikati ya Kijiji na sharti FDI ya kila siku irekebishwe kadri inavyopokelewa na Kamati.

Kuundwa kwa Kamati ya Usimamizi wa Moto ya Kijiji (KUMK)

KUMK ni sehemu muhimu ya UJM. Hivyo basi, Halmashauri za Vijiji zitachagua wajumbe wa KUMK ambao watahitaji kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Miongoni mwa sifa za Wajumbe ni kwamba watapaswa kutoka kila Kitongoji ndani ya Kijiji. Pia Wajumbe wa KUMK wanapaswa kuwa wakulima wenye uelewa na uzoefu wa moto wa nyika. KUMK itakuwa na wajumbe 25 watakaosimamia masuala yote ya UJM. Wajumbe hao watakuwa na wajibu wa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) ambao hata hivyo, ni lazima uidhinishwe na Mkutano wa Kijiji. Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) utaongoza Wajumbe wa KUMK katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Moto Kijijini (MUMK)

MUMK ni waraka unaotoa miongozo ya kimbinu kwa KUMK ili kuiwezesha kufikia matokeo ya UJM kwa kipindi cha miaka mitano. Shughuli zote za UJM na majukumu yanayoambatana na shughuli hizo, yameandikwa katika MUMK. Kwa kawaida, Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) unatoa bajeti ya miaka mitano ya utekelezaji wa mpango pamoja na mapendekezo ya namna bora ya kupata fedha. “MUMK cha Kidete” ni mfano wa Mpango wa Usimamizi wa Moto ambao unaweza kutumika kama jukwaa la kuandika Mpango wa Usimamizi wa Moto kwa Vijiji vyote.

Kuanzishwa kwa Kikosi cha Kuzima Moto Kijijini (KKMK)

KKMK ni timu yenye watu angalau 15 walio na utimamu wa mwili ambao wamefunzwa kuzima moto kwa usalama na kwa ufanisi. Kiongozi wa KKMK aliye na ujuzi wa uongozi, maarifa, na uzoefu atasimamia timu na kuchukua udhibiti wa shughuli za timu. Hata hivyo, Kijiji kinaweza kuwa na KKMK zaidi ya kimoja kulingana na ukubwa wake au jiografia yake. Hivyo basi, KUMK itakuwa na jukumu la kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kuzimia moto vinavyohitajika pamoja na kusimamia shughuli za KKMK.

Kikosi cha Kuzima Moto Kijijini (KKMK) kitapaswa kuwa katika hali ya utayari wakati wowote pindi kunapokuwa na hali mbaya ya hewa ya moto au iwapo viwango vya FDI vitakuwa juu zaidi ya 55. Iwapo KUMK itaona inafaa, inaweza kukishauri KKMK kusaidia wananchi wenye vibali vya moto katika shughuli zao za uchomaji. Hata hivyo, ili KKMK kifanye shughuli zake kwa usalama na ufanisi mzuri, vifaa vya kinga binafsi, zana na vifaa kama vilivyoorodheshwa kwenye jedwali 1 vinapaswa kutolewa kwa KKMK.

Jedwali 1: Vifaa muhimu vinavyopendekezwa kwa ajili ya KMKK

Aina ya kifaa	Idadi	Makisio ya gharama	Jumla ya makisio ya gharama (TZS)	Jumla ya makisio ya gharama (Euro)
Ovaroli za pamba	15	150,000	2,250,000	878
Viatu vya Ngozi	15	100,000	1,500,000	585
Kofia za kitambaa cha pamba	15	60,000	900,000	351
Kinga za mikononi za ngozi (gloves)	15	11,500	172,500	67
Miwani ya kuinga macho	15	20,000	300,000	117
Mipira ya kuzimia moto	12	28,000	336,000	131
Shanta (mabomba) za kuzimia moto	4	278,000	1,112,000	434
Reki-jembe	4	30,000	120,000	47
Panga	2	20,000	40,000	16
Kisambazia matone ya moto	1	120,000	120,000	47
Uma wa kuvutia majani	6	15,500	93,000	36
Kijiti cha kuwashia/ kusambazia moto	4	3,000	12,000	5
Sanduku la huduma ya kwanza (lenye vifaa vya kutibia majeraha ya moto)	1	200,000	200,000	78
Jumla ya gharama (TZS) & (Euro)			7,155,500	2,792

Uanzishwaji wa Mfuko wa Moto wa Vijijini

Mfuko wa Moto wa Kijiji (MMK) upo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa MUMK. Kwa muktadha huu, KUMK itasimamia utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji pamoja uendeshwaji wa Mfuko wa Moto wa Kijiji (MMK). Kimsingi, mfuko huo utapatikana kutokana na ada za kila mwaka zinazolipwa na wawekezaji wenye mashamba ya miti kutoka nje ya Kijiji. Kwa kuongezea, mfuko huo pia utatunishwa kwa michango mbalimbali pamoja na ufadhili.

Fedha za mfuko zitatumika kwa mujibu wa MUMK. Kwa kawaida, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya maandalizi ya barabara za Kijiji za kuzuia moto, kununua zana za kuzimia moto, matumizi ya dharura wakati wa kuzima moto, kununua vifaa vya kinga ya kibinafsi, kugharamia usafiri wakati wa (mikutano na mafunzo), na posho kwa ajili ya walenzi wa Kikosi cha kuzima moto.

Usimamizi wa MMK unapaswa kuwa wa uwazi na utakabidhiwa na kusimamiwa na watu mahususi ambao watawajibika kwa ajili ya mapato au matumizi yoyote ya mfuko. Kimsingi, MMK unapaswa kuwa na akaunti yake ya benki inayojitegemea ambayo itaendeshwa kwa mujibu wa mfumo wa serikali. Hata hivyo, iwapo kibali cha kufungua akaunti ya benki inayojitegemea kitashindikana kutokana na taratibu za sera za fedha, ni sharti Mwenyekiti wa KUMK awe miongoni mwa watu wanaotakiwa kuidhinisha matumizi ya fedha za mfuko. Sambamba na hilo, KUMK itapaswa kuchagua Mweka hazina kutoka miongoni mwa wajumbe wa KUMK ambaye atawajibika katika kuweka kumbukumbu za kila siku za mapato na matumizi ya mfuko wa moto kulingana na matakwa ya MUMK.

Mahesabu ya MMK yatabainishwa na ukaguzi wa kila mwaka wa shughuli za UJM ambao utajumuisha wasimamizi wa mfuko. Taarifa ya fedha ya kila mwaka ya mfuko itawasilishwa kwa

Halmashauri ya Kijiji na hatimaye kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Wawekezaji hai ambao wanalipia ada zao za kila mwaka watapewa taarifa za kila mwaka za mfuko wa moto na ripoti ya ukaguzi wa shughuli za UJM.

Kupanga na kuimarisha mifumo ya barabara za kuzuia moto

Ni muhimu kupanga na kuainisha barabara za kuzuia moto ambazo zitasaidia kulinda mali za Kijiji kutokana na moto. Barabara za kuzuia moto pia zitazua kuenea kwa moto unaoanzia ndani ya Kijiji na kuenea hadi Vijiji vya jirani. Barabara za kuzuia moto ni lazima zitayarishwe kwa wakati maalum na kwa vipimo sahihi ili kuwa na ufanisi unaotakiwa.

Kwa vile utayarishaji wa barabara za kuzuia moto unaweza kuendelea hadi msimu wa kiangazi, itakuwa muhimu kuweka kipaumbele kwa barabara za kuzuia moto ambazo zinapaswa kutayarishwa kwanza. Barabara za kuzuia moto zinapaswa kutoa ulinzi zaidi kwa maeneo yenye hatari kubwa ya kutokea kwa moto.

Mwanzoni mwa msimu wa kiangazi na wakati wa kilele cha msimu wa moto, barabara zote za kuzuia moto zinapaswa kuwa zimetayarishwa. Hata hivyo, baadhi ya maeneo yenye unyevunyevu na mabonde ambayo kwa kawaida, huchelewa kukauka na kuwaka yataondolewa kwenye sheria hii. Hivyo basi, hakuna kuchoma moto kunakopaswa kuruhusiwa kuanzia mwezi Oktoba hadi mvua ya kwanza inpoanza kunyesha. Marufuku hii ya kuchoma moto inapaswa kutekelezwa bila kisingizio chochote.

Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK) cha Kidete unatoa mfano mzuri wa mpango wa usimamizi wa moto wenye barabara za kuzuia moto zenye vipimo maalum.

Uanzishwaji wa miundombinu ya kimkakati

Barabara, vituo vya maji, vifaa vya kudhibiti moto na barabara za kuzuia moto kwa wastani ni ghali kuanzishwa, lakini miundombinu hiyo tajwa hapo juu, inahitajika ili kuboresha shughuli za UJM ndani ya Vijiji. Kwa bahati nzuri, wananchi wataingia gharama hizi mara moja tu wakati wa mwaka wa kwanza wa utekelezaji na hazitarudiwa tena kila mwaka. Hivyo basi, juhudi za pamoja zinahitajika ili kifadhili jambo hili muhimu.

Kutoa vibali vya kutumia moto kwa kutekeleza vigezo vya uchomaji moto salama

Wamiliki wa mashamba, warina asali, wachoma matofali, wachoma mkaa na wapasuaji wa mbao kwa kutumia mashine za Ding-dong, au mtu yeyote ambaye atakuwa akitumia moto wa wazi ndani ya mipaka ya Kijiji ni lazima apate kibali kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa mujibu wa sheria Ndogo za Kijiji za kuzuia na kusimamia moto. Madhumuni ya kibali hiki ni kuhalalisha na kudhibiti matumizi holela ya moto.

Afisa Mtendaji wa Kijiji ni lazima aweke kumbukumbu ya vibali vyote vilivyotolewa kwenye rejista ya vibali vya moto. Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri (MMM) atapaswa kupokea ripoti ya kila mwezi ya vibali vilivyotolewa. Rejea "Sheria Ndogo za Kuzuia na Kusimamia Moto za Halmashauri za Vijiji" namna zinavyoelezea utoaji wa vibali vya kutumia moto.

Mazingira wezeshi ya kutekeleza sheria Ndogo za moto

Nchini Tanzania, sheria Ndogo zinatungwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Sheria hii inaruhusu Wilaya, Miji, Manispaa, Halmashauri za Miji na Vijiji kupitisha sheria Ndogo ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Kwa kurejelea sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto zilizokuwepo, Mradi wa Pandamiti Kibiashara uliunganisha juhudi na Mwakili wa serikali za Wilaya na Mikoa pamoja na wataalam wa masuala ya moto wa misituni ili kuandaa rasmu ya "Sheria Ndogo za Kuzuia na Kusimamia Moto wa Halmashauri za Vijiji". Rejea rasimu ya Sheria Ndogo za Kuzuia na Kusimamia Moto za Halmashauri za Vijiji.

Iwapo sheria Ndogo za Kijiji zitatungwa kama zilivyowasilishwa kwenye rasimu hii, zitatoa misingi ya kisheria ya kina kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UJM kama vile KUMK, KKMK, MUMK,

MMK, FDI, na nama bora ya kutoa vibali vya kuchoma moto. Zaidi ya hayo, zitafafanua makosa ya moto na adhabu zinazohusiana na makosa hayo.

Rasimu ya sheria Ndogo inapaswa kupitiwa na kuhodhiwa na Halmashauri ya Kijiji na baadaye kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji ili kujifariji iwapo rasimu hiyo inakidhi matakwa yao ya msingi na kwa namna ya kipekee, kuona kama inazingatia mahitaji ya msingi ya UJM.

Kutekeleza mifumo ya kuripoti

Kutunza kumbukumbu kama vile (Ripoti za uchunguzi wa moto, utoaji wa vibali, kutoza faini, na maendeleo ya kazi) ni njia nzuri sana ya kupima mafanikio ya shughuli za UJM. Ripoti hizo zitaifahamisha KUMK kuhusu maendeleo ya shughuli mbalimbali za usimamizi wa moto Kijijini kama vile utayarishaji wa barabara za kuzuia moto, matukio ya moto na maendeleo ya utayarishaji wa mashamba. Ripoti zote zinapaswa kuwasilishwa kwa MMMH ambaye atapaswa kupokea na kutayarisha ripoti ya Halmashauri yote na kuituma kwa Mkuu wa Wilaya na Mratibu wa Moto wa Msituni wa Mkoa (MMMM).

1.2.2 Kuzuia

Kuzuia kunafafanuliwa kama kutambua sababu za moto na kutekeleza hatua za kuziondoa au kuzipunguza.

Uzoefu unaonyesha kwamba rasilimali chache za kukabiliana na masuala ya moto zinazopatikana Kijijini hasa hutumiwa katika ulinzi na kuzima moto. Kutokana na uzoefu huo, imebainika kwamba uzuiaji kama miongoni mwa mkakati wa kudhibiti moto hautumiki sana Vijijini. Hivyo basi, iwapo mkakati huu utatekelezwa kwa ufanisi, una uwezekano wa kuwa na matokeo mazuri katika kuzuia hasara za moto wa nyika. Mkakati wa kuzuia moto unaweza kugawanywa katika makundi matatu kama yafuatavyo:

(i) Mafunzo na uhamasishaji (ii) kuondoa/kupunguza viwako msituni na (iii) utekelezaji wa sheria unaochwenda sambamba na upangaji wa matumizi bora ya ardhi na kujenga uwezo.

Uchambuzi wa hatari ya moto ni hatua nzuri ya kuanzia katika kutekeleza mkakati wa kuzuia moto. Kwa sababu uchambuzi wa hatari ya moto unapaswa kufichua vyanzo vya moto pamoja na maeneo yaliyo hatarini zaidi kushika moto.

- **Mafunzo na uhamasishaji:** Makundi yanayohitaji kuelimishwa na kuhamasishwa kuhusu athari hasi za moto wa nyika ni pamoja na: viongozi, vijana, umma kwa ujumla wake na vyombo vya habari. Aidha, KKMK kinapaswa kupata mafunzo ya kila mwaka ya mbinu za msingi za kuzima moto. Pia ni vyema KUMK iwezeshe kupata ujuzi juu ya masuala ya moto kwa ujumla wake na kuwezesha kupata ujuzi wa kiutawala utakaoweza kusimamia na kuongoza shughuli za usimamizi wa moto ndani ya Vijiji. Maafisa ugani wa Vijiji waliowezeshwa pia wanapaswa kutoa mafunzo na uhamasishaji kupitia mbao za maonyesho ya FDI, shughuli za shuleni, mikutano, majukwaa ya vyombo vya habari pamoja na kutoa mafunzo rasmi.
- **Ujenzi wa miundombinu** (kama vile barabara za kuzuia moto, barabara, vituo vya maji, n.k.): Baada ya kutambua maeneo hatarishi ndani ya Kijiji kwa kutumia uchambuzi wa hatari ya moto (wepesi wa maeneo hayo kushika moto na idadi ya vichomaji katika maeneo hayo), ni lazima hatua zitekelezwe ili kuzuia moto kuanza katika maeneo haya. Hii inaweza kujumuisha kuweka barabara za kuzuia moto, kuboresha miundombinu kama vile barabara na vituo vya maji, au kufikiria upya namna bora ya kutumia moto kwa watu wenye mazoea ya kuanzisha moto usiohitajika. Miongoni mwa shughuli zinazoweza kufanyika ili kuzuia kuanza kwa moto usiohitajika ni pamoja na (kutenga shughuli hatarishi kama vile uzalishaji wa mkaa, moto wa kupikia na moto kwa ajili ya kuandalia mashamba). Vilevile, wapasuaji wa mbao kwa kutumia mashine zinazohamishika ni sharti wawajibike katika kutawanya taka zitokanazo na upasuaji wa mbao ili zisiwe miongoni mwa vyanzo hatarishi vya moto Kijijini. Kwa lugha nyingine ni kwamba, hairuhusiwi kuweka malundo makubwa ya taka zitokanazo na upasuaji wa mbao kwa sababu malundo hayo yakipata moto ni vigumu kuzimika.

- **Utekelezaji:** Watu binafsi au vikundi vya watu wanaokiuka au kuacha kutimiza majukumu yao, wanapaswa kuwajibishwa. Sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto zimetangazwa ili kuwalinda Watanzania pamoja na mali zao dhidi ya moto usiohitajika. Kwa kawaida, sheria Ndogo za Vijiji za kuzuia na kusimamia moto zinatungwa na kukubaliwa na wanakijiji wenyewe, na kuna adhabu kwa wale ambao watashindwa kuzingatia sheria hizo. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zinazozuia utekelezaji mzuri wa sheria hizo ni kutokujali kwa baadhi ya wanavijiji. Pia uwezo na utashi wa kisiasa wa kusimamia sheria hizo mara nyingi haupo. Hivyo basi, dhana ya uwajibikaji ni sharti ijengwe miongoni mwa wanajamii kupitia utekelezaji wa sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto.

Mfano mzuri wa uwajibikaji ni kwamba, Kijiji kinaweza kuamua mahali ambapo watu wanaruhusiwa kujenga nyumba na kuishi, au mahali ambapo barabara za kuzuia moto zinapaswa kuwekwa. Baada ya watu kukubaliana, tamko hilo linapaswa kusimamiwa na Mamlaka husika. Kwa kufanya hivyo, Mamlaka hiyo itakuwa inaonyesha dhana ya uwajibikaji kwa jamii yake.

- **Upangaji wa matumizi bora ya ardhi:** Upangaji mzuri wa matumizi bora ya ardhi utahakikisha kuwa miundombinu ya kuzuia moto inajengwa mahali ambapo itakuwa na athari ndogo katika mazingira, kutoa manufaa ya hali ya juu kwa watumiaji wa ardhi na kuhakikisha usalama wa wanavijiji. Mifano ya miundombinu inayochangia uwepo wa usalama wa moto ni pamoja na: - uwekaji wa barabara za kuzuia moto, uanzishaji wa vituo vya maji, ujenzi wa barabara, ujenzi wa nyumba za shule na majengo mengine pamoja na kutenga maeneo ya uchomaji mkaa na matofali. Upangaji wa matumizi bora ya ardhi ni lazima ufanyike kupitia timu za Wilaya za usimamizi wa matumizi bora ya ardhi na zinapaswa kushauriana na wataalam wa moto.
- **Bajeti:** Masuala yote ya UJM yanahitaji mchango wa kifedha. Kwa hiyo, usimamizi wa mfuko wa moto wa Kijiji ni muhimu sana kwa sababu utakuwa chanzo pekee cha fedha. Hivyo basi, ni muhimu kuhakikisha kwamba wawekezaji wanalipa ada zao za kila mwaka na kwamba, fedha katika mfuko huo zinasimamiwa vizuri. Ni vyema mfuko wa moto uwe na akaunti ya benki inayojitegemea ili iwe rahisi kuratibu uwazi pamoja na uwajibikaji kwa viongozi wa mfuko. Shughuli zote zinazopangwa kufanyika ni sharti ziwekewe bajeti ya kila mwaka.

1.2.3 Kuzima

Neno kuzima moto linaweza kufafanuliwa kama matayarisho yote yaliyofanywa, hatua zilizochukuliwa, nyenzo zilizotumiwa kudhibiti moto, namna moto ulivyopunguzwa makali yake, kulindwa na hatimaye chanzo na madhara yake kuchunguzwa. Hii inamaanisha kwamba, kabla ya tukio la moto kulikuwa na maandalizi yaliyofanywa ambayo yatahakikisha mwikikio mzuri kwenye moto, vitendo wakati wa tukio la moto ambavyo vitaamua matokeo ya juhudi za kuzima moto na shughuli zitakazofuata baada ya moto kudhibitiwa, ambavyo vitachangia kuongeza ufanisi wa kuzima moto na kuzuia kutokea tena kwa moto.

Moja ya vigezo muhimu vya kuzima moto kwa ufanisi ni uharaka wa kukabiliana na moto wenyewe. Ufanisi katika masuala ya kuzima moto ni pamoja uwepo wa vitendo vilivyoratibiwa vya kuleta rasilimali sahihi na kutoa taarifa sahihi za moto usiohitajika bila kuchelewa.

Ili kuwa na uwezo wa kukabiliana na moto, sehemu moto ulipo ni sharti liljulikane haraka iwezekanavyo. Mara tu eneo la moto linapojulikana, rasilimali (watu na zana) zinazohitajika kudhibiti moto ni lazima ziwe karibu. Kwa hiyo, ni muhimu kuandaa na kusimamia upatikanaji wa rasilimali. Hata hivyo, ni lazima kuwe na timu ya kuzima moto iliyo katika utayari wa kufanya kazi ya kuzima moto wakati wowote iwapo FDI itakuwa juu zaidi ya 55. Pia, kama kutakuwa na tukio la moto, ni lazima Kikosi kiwe na njia ya kukiwezesha kufika kwenye eneo la moto ndani ya muda mfupi iwezekanavyo.

Vitendo vyote vya kuzima moto ni lazima vizingatie hatari ya moto ya siku hiyo. Ikiwa hali ya hewa ni ya joto, kavu, na upepo (FDI zaidi ya 55), Kikosi cha Kijiji cha kuzima moto ni sharti kiwe katika tahadhari ya hali ya juu na maamuzi yake ya kukabiliana na moto ni lazima yawe ya haraka sana.

Mpangokazi wa Kijiji wa kusimamia Moto (MKKM) utaelekeza kila mwanakijiji hatua za kuchukua katika hali tofauti za FDI. MKKM ni sehemu ya Mpango wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji (MUMK). Mpangokazi unatoa maagizo kwa watu maalum wanaohusika na ulinzi wa moto, uzuiaji na shughuli za kuzima moto. MKKM kwa kawaida hulenga shughuli za kuzima moto ambazo zinaendana na ukadiriaji wa FDI ya siku hiyo. Umuhimu wa Mpangokazi ni kwamba utaboresha shughuli kama vile kuzima moto na kuwezesha utekelezaji wa majukumu kama vile utayarishaji wa barabara za kuzuia moto kwa wakati. Jedwali la 2 linaonyesha Mpangokazi wa Kijiji wa Kusimamia Moto.

Wakati wa hali ya juu ya FDI, viwako vinavyotoa moshi ndani ya maeneo ambayo moto ulitokea, vinaweza kuwaka kwa urahisi. Kwa hiyo, maeneo yaliyochomwa moto ni lazima yafanyiwe doria na ulinzi mpaka eneo litakapokuwa salama.

Mwisho, uchunguzi wa moto ni sharti ufanywe ili kubaini kilichosababisha moto huo na pia kutathmini ufanisi wa shughuli za kuzima moto ili kubaini kama taratibu bora za usimamizi wa mashamba (kama vile upunguzaji wa miti, upogoaji wa matawi na kuweka barabara za kuzuia moto) zilifuatwa kama zinavyofafanuliwa kwenye agizo la kiufundi nambari 1 la Wizara ya Maliasili na Utalii la mwaka 2021. Matokeo ya uchunguzi wa moto yanapaswa kuweka misingi bora ya utekelezaji wa hatua za kuzuia kutokea kwa moto na kuufungulia mashitaka upande unaohusika na moto huo.

Jedwali 1: Mpangokazi wa Kijiji wa Kusimamia Moto

HATUA ZA TAHADHARI YA MOTO	RANGI YA BLUE	RANGI YA KIJANI	RANGI YA NJANO	RANGI YA CHUNGWA	RANGI NYEKUNDU
FDI	0 - 20	21 - 45	46 - 60	61 - 75	75 – 100
Tabia ya Moto	SALAMA	WASTANI	HATARI	HATARI SANA	HATARI KUPINDUKIA
Urefu wa ndimi za moto	0 - 1m	1 – 1.2m	1.2 – 1.8m	1.8 – 2.4m	2.4m au zaidi
Kamati ya Usimamizi wa matumizi bora ya moto	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Kuwasilliana na wanakijiji juu ya alama ya FDI na kuangalia kama alama ya FDI inazidi 55 .	Toa katazo la matumizi ya moto kabisa, pia weka kikosi cha moto, wananchi na mashuke katika hali ya tahadhari	Toa katazo la matumizi ya moto kabisa, pia weka kikosi cha moto, wananchi na mashuke katika hali ya tahadhari
Kikosi cha kupambana na moto	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Kiongozi wa kikosi na wanakikosi wachukue tahadhari ya moto	Kikosi kifike kwa kiongozi mkuu ndani ya dakika 10 kikiwa na mavazi rasmi na vifaa vya kuzimia moto	Kikosi kifike kwenye uwanja wa kukutania kikiwa kwenye mavazi rasmi na vifaa vya kuzimia moto
Kikosi cha kuangalia moto kutokea umbali mrefu	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Hakuna tahadhari yeyote ya kuchukua	Kama alama ya FDI itafikia 55 , sharti kikosi cha kuangalia moto kiendelee na majukumu yake	Kikosi cha kuangalia moto kiendelee na majukumu yake	Kikosi cha kuangalia moto kiendelee na majukumu yake kwa tahadhari sana kwa muda wa masaa 24
Wanakijiji	Waendelee na majukumu yao ya kawaida	Waendelee na majukumu yao ya kawaida	Kama alama ya FDI itafika 55 , hakuna ruhusa kuwasha moto maeneo ya wazi	Hakuna moto wowote wa wazi ambao utaruhusiwa kuwashwa isipokuwa tu kwa kibali maalum	Hakuna moto wowote wa wazi au Shughuli zozote hatarishi kwa moto ambazo zitaruhusiwa

1.2.4 Ukarabati

Baada ya moto kutokea, eneo lililoungua litahitaji kukarabatiwa. Hata hivyo, hatari kubwa na ya haraka ambayo inaweza kutokea katika eneo lililoungua moto ni mmomonyoko wa udongo. Katika shamba la miti lililoungua, upandaji mpya wa miti unapaswa kufanywa. Hata hivyo, kabla ya kupanda tena, eneo hilo linapaswa kuandaliwa vizuri. Miongoni mwa shughuli muhimu sana za kufanya ni pamoja na usimamizi wa viwako kama vile kuvitawanya au kuviondoa kabisa.

Kushindwa kusimamia uondoaji wa viwako katika maeneo yaliyoungua, siyo tu kwamba kutaleta hatari ya moto tu, bali pia kutapunguza eneo kwa ajili ya kuotesha miche upya (kwa sababu ni vigumu kuotesha miche kwenye malundo ya maranda).

1.2.5 Utafiti

Ubunifu na teknolojia mpya inayotumika katika usimamizi wa moto Tanzania, inapaswa kurithiwa na wamiliki wa mashamba. Kwa hiyo, Maafisa ugani ni sharti waandaliwe katika hali ya utayari ili wawekeza juhudi zao katika kutoa mafunzo na elimu kwa wanavijiji.

Aidha, wasomi wanaofanya utafiti kuhusu masuala yanayohusiana na moto, wanapaswa kuhimizwa kutafiti changamoto za moto katika maeneo hayo ili kutoa suluhu zinazowezekana.

Utunzaji wa kumbukumbu za shughuli za usimamizi wa moto hutengeneza msingi wa takwimu ambao utatoa taarifa ambazo zinaweza kutumia na wasimamizi wa moto kufanya maamuzi bora. Rejesta zinazopaswa kuhifadhiwa ni pamoja na : Ukadiriaji wa FDI, rejesta ya utoaji wa vibali, rejesta ya matukio ya moto, faini za moto zilizopokelewa, rejesta ya michango ya wawekezaji, rejesta ya zana, rejesta ya matukio ya moto, nk.

Ukaguzi wa kila mwaka wa shughuli za usimamizi wa moto utatoa mrejesho kwa Kamati ya usimamizi wa moto kuhusu mapungufu yaliyopo katika mikakati yao ya usimamizi na kwa hivyo, kutafuta fursa za kuboresha.

2. UCHAMBUZI WA MAENEO HATARISHI YA MOTO

Lengo la uchambuzi wa maeneo hatarishi ya moto ni kutambua maeneo ambayo yataathiriwa sana na moto usiohitajika endapo utatokea. Hivyo basi, maeneo yaliyo kwenye hatari kubwa ya moto kutokea yanapaswa kupewa kipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za usimamizi jumuishi wa moto .

Mafanikio ya shughuli za usimamizi jumuishi wa moto yanategemea tathmini ya hatari ya moto iliyofanywa katika eneo lililoathiriwa na moto usiohitajika na kutambua maeneo ya kipaumbele cha hatari ya moto. Uchambuzi wa maeneo hatarishi ya moto unapaswa kufanyika katika ngazi ya Kijiji na zaidi ya hayo, uchambuzi huo pia unapaswa kufanyika katika ngazi ya Wilaya. Uwepo wa mazao yenye thamani ya juu kama vile mashamba ya miti ya kupandwa na rekodi za matukio ya moto katika maeneo ya jirani na mazao hayo yenye thamani ya juu itakuwa ni sehemu nzuri ya kuanzia katika kubainisha maeneo hatarishi ya moto.

Matokeo ya uchambuzi wa maeneo hatarishi ya moto yatasaidia Mamlaka kuweka kipaumbele katika maeneo yenye hatari kubwa ambapo shughuli za usimamizi jumuishi wa moto zitafanyika ili kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa.

3. MAJUKUMU NA WAJIBU WA VIONGOZI WA SERIKALI

Wajibu wa viongozi wa serikali katika kufanikisha utekelezaji wa mfumo wa UJM ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kimkakati katika nyanja za uongozi, uwezesaji na mbinu za utekelezaji. Katika suala hili kuna majukumu kadhaa ambayo yanapaswa kutimizwa ndani ya nyanja tofauti za kiutekelezaji za serikali kama ifuatavyo:

3.1 Majukumu ya Serikali ya Kuu

- Kuidhinishwa kwa mfumo wa shughuli za UJM ndani ya maeneo hatarishi nchini.
- Kuratibu na kutoa usaidizi katika udhhibiti wa moto.
- Kutoa msaada wa kifedha, rasilimali watu pamoja na kujenga uwezo.
- Kukuza uwezo wa taasisi za mafunzo kwenye suala la UJM
- Kuwezesha matangazo ya Kitaifa kujumuisha uhamasishaji wa shughuli za usimamizi jumuishi wa moto na maonyo kuhusu FDI.
- Taasisi za utafiti (TAFORI, TARI) kujihusisha na shughuli za UJM
- Kuendeleza na kundumisha mahusiano na taasisi za Kimataifa zinazojihusisha na masuala ya moto.
- Ukusanyaji na uchanganuzi wa takwimu za hali ya hewa zilizopatikana kwa njia ya setilaiti na kutoa taarifa za FDI katika Vijiji husika.
- Kufanya shughuli za UJM kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira) na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

3.2 Majukumu ya Serikali ya Mkoa

- Kuwasilisha masuala ya kipaumbele ya shughuli za UJM (kama vile kuajiri na kuwajengea uwezo watumishi wa ugani, sheria ndogo za kuzuia moto, kupata na kuwasilisha takwimu za FDI vijijini).
- Kuwasilisha hitaji la dharura la kuweka kipaumbele katika misitu kama sekta muhimu ya kiuchumi kwa maendeleo na kuweka kipaumbele katika uwekezaji upya.
- Kuteua Mratibu wa Moto wa Msituni wa Mkoa (MMMM) kwa ajili ya kufuatilia na kuripoti maendeleo ya shughuli za usimamizi jumuishi wa moto.
- Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa misitu kibiashara katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vijiji.
- Kukuza uwekaji wa viwango katika vipengele muhimu vya UJM kati ya wilaya na vijiji vyote vinavyotekeleza UJM
- Kufanya shughuli za UJM kuwa ajenda ya kudumu kwenye mikutano yote ya Mikoa.

3.3 Majukumu ya Serikali ya Wilaya

- Kuteua Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri (MMMH) mwenye moyo wa kutimiza majukumu yake hasa (anayeweza kupimwa kwa viashiria muhimu vya utendaji) kufuatilia na kuripoti maendeleo ya shughuli za UJM kwa Mamlaka husika yaani MMMM. Aidha, kuwa mtu wa mawasiliano kwa ajili ya kutatua changamoto za masuala ya shughuli za UJM kutoka vijijini.
- Kusaidia uanzishwaji na uendeshwaji wa MMK kama unavyotamkwa kwa mujibu wa sheria Ndogo za kuzuia na kusimama moto.
- Kuendeleza huduma makini za ugani na mafunzo juu ya shughuli za misitu na kuzuia moto katika Vijiji ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa MUMK, mafunzo kwa KKMK na KUMK.
- Kufanya tathmini ya kila mwaka ya hatari ya moto wa msituni katika Halmashauri.
- Kuendeleza uwezo halmashauri wa kuzima moto ili kukabiliana na maafa ya moto.
- Kudhibiti shughuli zote za moto katika Vijiji kupitia tathmini/ukaguzi na kufuatilia makosa katika usimamizi/matumizi ya moto katika Vijiji.
- Kusaidia katika kuweka miundombinu ya kuzuia moto katika Vijiji (vituo vya maji, barabara, na miundombinu nyingine za kuzuia moto).
- Kusaidia Vijiji kupata takwimu za FDI za kila siku wakati wa msimu wa moto.
- Kufanya shughuli za UJM kuwa ajenda ya kudumu katika Mikutano yote ya Halmashauri.

3.4 Majukumu ya Serikali ya Kata

- Kusuluhisha migogoro ya kiutendaji kati ya Vijiji na wanakijiji.
- Kuratibu mikutano ya KUMK
- Kuwasilisha taarifa za muda halisi juu ya moto wa nyika katika Vijiji.
- Kusaidia utekelezaji wa shughuli za UJM kwa ujumla wake.
- Kujenga uwezo wa Maafisa Kilimo wa Kata na Maafisa ugani wa Misitu katika shughuli za UJM ili wawe washauri wazuri kwa KKMK na KUMK. Rejelea sheria Ndogo za moto kuzuia na kusimamia moto.
- Kufanya shughuli za UJM kuwa ajenda ya kudumu katika mikutano yote ya Mabaraza ya Kata.

3.5 Majukumu ya Serikali ya Kijiji

- Kuunda na kuimarisha MUMK ukiambatanishwa na Mpangokazi wa Kijiji wa Kusimamia Moto (MKKM).
- Kutumia MUMK kama mwongozo wa kutekeleza UJM ndani ya Kijiji.
- Kuendeleza na kutekeleza sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa msituni.
- Kupeleka kesi maalum Katani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.
- Kuhamasisha wamiliki wa mashamba kuandaa barabara za kuzuia moto kwa mujibu wa
- Kuwezesha mafunzo ya moto na kufanya uhamasishaji ndani ya Kijiji.
- Kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika (Kusimamia mfuko wa moto wa Kijiji, kutoa vibali vya uhomaji moto, kutumia takwimu za FDI , kukusanya michango kutoka kwa wawekezaji wa nje ya Kijiji, kusimamia kazi za KUMK na KKMK, kufanya uchunguzi wa moto, kutoa taarifa kwa MMMH kupitia kwa uongozi wa Kata na kudhibiti matumizi ya moto miongoni mwa: warina asali, wachoma mkaa , wachoma matofali na wapasuaji wa mbao).
- Kununua, kukarabaiti au kutengeneza zana za kudhibiti moto.
- Kufuatilia na kuripoti masuala yanayohusiana na moto kwa MMMH.
- Kusaidia wanakijiji katika kutumia mbinu bora za usimamizi wa mashamba makubwa ya miti ikiwa ni pamoja na kupunguzia miti, kupogolea matawi na kuweka barabara za kuzuia moto kwa ajili ya kutimiza lengo la jumla la kupunguza viwako msituni.
- Kufanya mkakati wa UJM kuwe ajenda ya kudumu katika mikutano yote ya halmashauri za Vijiji.

4. MAELEZO YA MWISHO

Katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania, sekta ya misitu ndiyo chanzo kikubwa cha mapato ya serikali. Kwa muktadha huu, ni jambo la busara kusema kwamba sekta ya misitu pia ni kichocheo muhimu zaidi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Kanda hiyo kwa sababu misitu inazalisha fursa na ajira nyingi. Pia misitu inazalisha uwiano chanya wa kibiashara kwa sababu mazao mengi ya misitu yanauzwa nchi za nje. Hivyo basi, kadiri tasnia hii ya misitu inavyokuwa na mafanikio, ndivyo ukuaji wa kiuchumi katika Kanda ya Juu Kusini mwa Tanzania unavyozidi kuongezeka. Kutokana na ukweli huo, serikali ina motisha ya kutosha ya kulinda na kuendeleza sekta ya misitu nchini.

Andiko la "Usimamizi Jumuishi wa Moto - Mwongozo kwa Mashamba ya Misitu ya Kibiashara", lililochapishwa mwaka 2019, linaonyesha mtazamo wa mapema wa serikali ya Kuu katika kutambua tatizo la moto. Maudhui ya waraka huo yanatokana na mwelekeo wa uchomaji moto misitu, sera zilizopo za Kitaifa ikiwa ni pamoja na sera ya misitu iliyofanyiwa marekebisho hivi karibuni, mapendekezo ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), na ongezeko la uwekezaji katika misitu midogo, ya kati na mikubwa ya kibiashara nchini (Macric, na Lyimo, 2019).

Uwekezaji katika mfumo wa UJM ndio nyenzo bora ya kusukuma ajenda ya maendeleo ya sekta ya misitu Tanzania. UJM ni mfumo wa Kimataifa ambao ni wa uhakika na umetoa mchango mkubwa kwa ustawi wa watu, afya ya mazingira, na kuzuia hasara zitokanazo na moto usiohitajika. Ijapokuwa utekelezaji wa mfumo huu unahitaji uongozi thabiti na usaidizi wa kifedha, lakini matokeo ya mfumo hutoa manufaa katika maeneo mbalimbali.

Kuzuia moto wa nyika usiohitajika sio tu kwamba huongeza mavuno ya mbao kwa wanavijiji, lakini pia huchochea maendeleo ya Kikanda kupitia ongezeko la mapato ya kodi. Faida zingine zitokanazo na sekta ya misitu katika ngazi ya chini kwa wananchi wa kawaida ni kama vile usalama wa Kijiji, uwepo wa wawekezaji kutoka nje ya Kijiji, upatikanaji wa ajira, ukuaji endelevu wa tasnia ya misitu, elimu na mafunzo bora, ubunifu, mauzo ya bidhaa za mbao nchi za nje na mazingira yenye afya bora.

Utekelezaji wa UJM utachukua muda kwa sababu Vijiji vingi viko hatarini kukumbwa na madhara yatokanayo na moto wa nyika. Pamoja na kwamba jitihada za kutekeleza UJM ikiwa ni pamoja na kuelimisha na kutoa mafunzo kwa wanavijiji, maofisa ugani, wakufunzi na maofisa wengine, lakini juhudi hizi ni kidogo sana. Hivyo basi, ili kuendeleza kasi ya uanzishwaji wa UJM, serikali haina budi kufanya jitihada za makusudi. Hata hivyo, iwapo vichocheo vya usimamizi jumuishi wa moto vitashindwa, juhudi zote zinazofanywa kutekeleza mfumo huo nazo zitatatizika.

UJM ni mfumo unaohitaji ushirikiswaji mpana kwa sababu kanuni zilizomo ndani yake zinahitaji ushiriki wa viongozi wa ngazi zote za serikali kuanzia Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji.

REJEA

- FAO 2006. Usimamizi wa Moto: Miongozo ya Hiari. Kanuni na Vitendo vya Kimkakati. Karatasi ya Kazi ya Usimamizi wa Moto Namba 17, Roma. Inapatikana kutoka www.fao.org/forestry/site/35853/en. Ilifikiwa: tarehe 22/09/2022.
- Fynbosfire. 2016. Kitabu cha Mwongozo wa Usimamizi Jumuishi wa Moto. Kuanzisha Vyama vya Ulinzi wa Moto nchini Afrika Kusini. Inapatikana kutoka A-Guide-to-IFM_Complete_Display.pdf (fynbosfire.org.za). Ilifikiwa: tarehe 22/09/2022.
- ITTO Shirika la Kimataifa la Mbao za Tropiki .Inapatikana katika Usimamizi Jumuishi wa Moto wa Misituni | ITTO | Shirika la Kimataifa la Mbao za Tropiki. Ilifikiwa tarehe 06/02/2023.
- Macric, S.A. na Lyimo, P.J. 2019. Miongozo ya Usimamizi Jumuishi wa Moto kwa Misitu ya Kibiashara Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Misitu na Nyuki.
- Myers, R. 2006. Kuishi na Moto: kuendeleza Mifumo Ikolojia na Riziki kupitia Usimamizi Jumuishi wa Moto. Tallahassee, Marekani. Mpango wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira wa Moto.
- Zietsman, J. na wenzake 2018. Mwongozo wa Kikanda wa SADC wa Usimamizi wa Moto wa Misitu. Toleo la 2.1. Inapatikana kwa: https://www.amis-fis.jp/hpffm/pdf/2_FFM_Guideline.pdf. Ilifikiwa tarehe 22/09/2022.



Indufor ...forest intelligence

NIRAS